

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Jumatano, 08 Mei 2019 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyе jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na C na maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi, simu za mikonomi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Ukurasa wa 1 kati ya 3

prof. exams.may19



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

- 1. Fafanua kwa kifupi athari nne za ongezeko la kasi la watu nchini Tanzania.
- 2. (a) Fafanua dhana ya mistari ya gridi,
(b) Kwa kutumia hoja tatu, onesha namna ambavyo mistari ya gridi ni muhimu katika usomaji wa ramani.
- ▲ 3. Toa tofauti nne kati ya majanga ya kiasili na majanga ya kibinadamu.
4. Eleza jinsi ambavyo matukio ya kinajimu yafuatayo hutokea:
 - (a) Kupatwa kwa juu
 - (b) Kupatwa kwa mwezi.
5. Ndege ya Shirika la Ndege la Emirates iliruka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es Salaam (45° Mashariki) saa 11:15 alfajiri kwenda Tokyo Japan (120° Mashariki). Je muda huo ilikuwa saa ngapi kwa saa za Japan? Onesha njia yako bayana.
6. Chambua kwa ufupi mafunzo manne yaliyotokana na vita vilivyopiganwa na Watanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani.
7. Kwa kifupi, changanua matokeo manne ya mkutano wa Berlin uliofanyika mwaka 1884/1885.
8. Elezea kwa kifupi changamoto nne za upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi katika nchi za Kiafrika baada ya uhuru.
9. Kwa kutumia hoja nne, tofautisha mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na wakati wa zama za chuma.
10. Kwa kutoa hoja nne, eleza kwa kifupi sababu zilizowafanya wananchi wa Tanganyika kuungana katika kudai uhuru wao.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika kila kipengele.

Kipengele cha I: Jiografia

11. Bainisha mambo manne yanayoathiri tabia nchi.
12. Eleza hatua tano zinazoweza kuchukuliwa na jamii ili kupunguza athari ikiwa janga la asili litatokea.

Ukurasa wa 2 kati ya 3

Kipengele cha II: Historia

13. Kwa kutumia dondoo tano, tofautisha mfumo wa utawala wa moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma uliotumika wakati wa utawala wa kikoloni.
14. "Mapinduzi ya viwanda yaliyotokea katika bara la Ulaya miaka ya 1760 hadi 1870 yalisababisha kuvamiwa na kugawanywa kwa Bara la Afrika". Tetea kauli hij kwa kutoa hoja tano.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

15. Eleza faida tano za matumizi ya kumbukumbu za upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia.
16. Fafanua stadi tano ambazo mwalimu wa Somo la Historia anapaswa kutumia ili kufundisha somo kwa weledi.